# SEREKALI Ya KIINGEREZA

# Na

# JIHADI

Na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

# SEREKALI YA KIINGEREZA
# NA JIHADI

Tafsiri ya Kiswahili ya: *Government Angreizī aur Jihād* (Urdu)

Mfasiri: Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani
Sura ya nje: Sharifu Tanwir Mujtaba

© Islam International Publications Ltd.
Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1900
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2019
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
S.L.P. 376, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

Cover design by: Salman Muhammad Sajid

ISBN: 978-1-84880-562-0
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# MAELEZO YA MWENEZI

## KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s., alizaliwa tarehe 13 Februari 1835 huko Qadian, India.

Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alijitolea kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi ya maana sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam

pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume s.a.w. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha mpango wa Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a.

## KUHUSU KITABU

Seyyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, alitumwa na Mwenyezi Mungu kubainisha mafundisho sahihi ya dini ya Kiislamu. Kwa lengo la kuelezea hakika ya jihadi alikiandika kitabu kimoja kiitwacho Government Angrezi aor Jihad,

(Serekali ya Kiingereza na Jihadi) kilichochapishwa mnamo tarehe 22 May 1900.

Katika kitabu hiki Seyyidna Ahmad a.s. alieleza hakika ya jihadi na hekima yake kulingana na Kurani, Hadithi na historia. Na alithibitisha kwamba katika siku za mwanzoni mwa Islamu, Waislamu kwa sababu ya kudhulumiwa na kuteswa sana waliruhusiwa kujitetea na kujilinda; waila Islamu ni dini ya amani na usalama. Na siku hizi vita vya dini havijuzu kabisa.

## SHUKRANI

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbasihiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania, aliyetumikia nchini Kenya na Ghana pia. Halafu Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Kenya, akaichunguza na kusahihisha tafsiri hii kwa uangalifu sana.

Aidha ndugu kadha wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal na

Sharifu Tanwir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin. Tafsiri hii ni tunda la Deski ya Kiswahili.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid
Rabwah. Pakistan
30.10.2011

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]
نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ[2]

# SEREKALI YA KIINGEREZA NA JIHADI

Falsafa ya masaala ya jihadi na uhakika wake hasa ni jambo la kutatanisha na ni habari ngumu kueleza, ambayo kwa kutokuielewa watu wa zama hizi na kadhalika wa zama za kati walifanya makosa makubwa makubwa. Nasi tunalazimika kukubali kwa aibu sana kwamba kwa sababu ya makosa hayo mabaya sana wapinzani wa Islamu walipata nafasi ya kushutumu dini takatifu ya Islamu ambayo ni kioo cha kanuni ya asili na inadhihirisha jalali ya Mungu Aliye hai.

Yapasa kujua kwamba neno jihadi limetokana na neno 'juhd', maana yake kutia bidii; kisha kimajazi likatumika kwa vita vya dini. Na inaonekana kwamba neno Yudd'h wanalotumia wahindu kumaanisha vita, kwa kweli pia ni Jihad lililogeuka-geuka. Maana, lugha ya Kiarabu ni mama wa lugha zote, na lugha zote zimetoka katika lugha hiyo, kwa hiyo, neno "Yudd'h"

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.
[2] Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

linalotumika katika lugha ya Kisanskriti kwa vita, kwa kweli ni 'Juhd' au "Jihadi", na kisha 'J' ikabadilishwa kuwa 'Y', na kwa kugeuzwa kidogo ikatamkwa kwa tashdidi.

Sasa tunataka kuandika jibu la swali hili kwamba kwa nini Islam iliihitaji jihadi, na jihadi ni kitu gani? Basi, ibainike kwamba Islamu ilipoanza tu ikakabili matatizo makubwa makubwa na mataifa yote yakawa maadui zake. Ilivyo kawaida ni kwamba Nabii au Mtume anapotumwa kutoka kwa Mungu na watu wanaiona Jumuiya yake kuwa ni kundi la watu wa kutumainiwa na wakweli na wenye bidii na wenye kusonga mbele, basi huzalika bughudha na husuda ya namna fulani katika mioyo ya mataifa na madhehebu ya zama hizo dhidi yao. Hususan, maulamaa na viongozi wa kila dini wanadhihirisha sana bughudha, kwani kwa sababu ya mtu huyo wa Mungu kudhihiri wanapungukiwa mapato yao na heshima zao. Wanafunzi wao na wafuasi wao huanza kutoka katika mtego wao. Kwani, wanazikuta sifa zote za imani na khulka na elimu katika mtu huyo anayedhihiri kutoka kwa Mungu. Hivyo, basi, wenye akili na busara wanaanza kutambau kwamba ile heshima waliyopewa hao wataalamu kwa kufikiria ujuzi wao na ucha-

Mungu wao na wema wao sasa hawastahiki kupewa; na majina ya heshima waliyopewa, kama vile Nyota ya Ummati, Jua la Ummati, na Sheikh wa masheikh na kadhalika, sasa hayafai kwao. Basi kwa sababu hizo wenye akili wanajitenga nao, kwani hawataki kupoteza imani zao. Basi, kwa kulazimika na kupata hasara hizo, kundi la maulamaa na masheikh limeendelea sikuzote kuwafanyia husuda manabii na mitume. Sababu yake ni kwamba katika zama za manabii na mitume watu hawa wanapata kuaibika sana, kwani kwa kweli hao ndio wneye nakisi na wana sehemu ndogo sana katika nuru. Na uadui wao kwa manabii na wakweli huwa kwa sababu ya ubinafsi tu. Na wanakula njama za kudhuru kwa kuzitii nafsi zao tu, bali wakati mwingine wanahisi katika mioyo yao pia kwamba kwa kumwudhi bila haki mtu mwenye moyo safi wameshikwa na ghadhabu ya Mungu. Na vitendo vyao pia wanavyoendelea kutenda kila wakati kwa kumpinga-pinga, vinaendelea kudhihirisha kwao hali ya moyo wao inayo hatia, lakini hata hivyo injini iendayo kasi ya moto wa husuda inaendelea kuwavuta kwenye mashimo ya uadui. Hizo ndizo sababu ambazo si tu ziliwanyima wataalamu wa washirikina, Mayahudi na Wakristo katika zama za Mtume s.a.w. kukubali haki, bali kuwachochea kufanya

uadui mkali. Kwa hiyo, wakahangaikia kuifutilia mbali Islam katika dunia kwa njia yoyote. Na kwa vile mwanzoni mwa Islamu Waislamu walikuwa wachache, kwa hiyo wapinzani wao kwa sababu ya majivuno yanayojikalia kitabia katika nyoyo na bongo za makundi kama hayo yanayojifikiria kuwa bora kuliko dhehebu jingine kwa mali, fedha, wingi wa idadi, na heshima na cheo, wakawafanyia uadui mkali Waislamu wa wakati huo, yaani masahaba. Na hawakutaka mmea huu wa mbinguni uimarike ardhini, bali walikuwa wakitumia nguvu zao zote kuwaangamiza wakweli hao, wala hawakuacha nafasi yoyote ya kudhuru. Na walikuwa na hofu isije dini hii ikaimarika na maendeleo yake yakasababisha maangamio ya dini yetu na taifa letu. Basi kwa hofu hiyo iliyojikalia mioyoni mwao kama tisho, wakafanya vitendo vya ukatili na dhuluma sana na wakawaua Waislamu wengi kikatili. Na kwa muda mrefu uliokuwa muda wa miaka kumi na mitatu waliendelea kufanya hivyo hivyo, na pasipo huruma waja waaminifu wa Mungu na fahari ya binadamu walikatwa vipande vipande kwa mapanga ya hao kina nduli wakorofi, na watoto mayatima na wanawake wanyonge na wadhaifu walichinjwa mitaani. Hata hivyo Mwenyezi Mungu akasisitiza kabisa kwamba

msishindane na shari, na vivyo hivyo wakafanya wakweli hao. Kwa damu zao mitaa ikawa myekundu, lakini hawakulalamika, wakachinjwa kama dhabihu lakini hawakutamka hata ah. Mtume Mtakatifu s.a.w. wa Mungu ambaye amani nyingi zisizohesabika zamfikia kutoka ardhini na mbinguni, akaloweka kwa damu mara nyingi kwa kupigwa mawe, lakini huyo mlima wa ukweli na uthabiti akastahamili mateso hayo yote kwa moyo mkunjufu na mapenzi. Lakini kwa njia hizo za kuonyesha subira na unyenyekevu, ukorofi wa wapinzani uliendelea kuzidi siku hadi siku, na wakaichukulia jumuiya hii takatifu kuwa windo lao. Ndipo Mungu ambaye hataki dhuluma na uonevu vipite kiasi ardhini Akawakumbuka watumishi wake waliodhulumiwa, na ghadhabu yake ikawashukia wenye shari , na kwa njia ya neno lake Takatifu, Kurani Tukufu, Akawapasha habari watumishi wake waliodhulumiwa kwamba kila mnachotendewa naviona vyote. Mimi, kuanzia leo, nawaruhusuni kushindana nao, na mimi ndimi Mungu Mweza sitawaacha wadhalimu bila kuwaadhibu. Hii ilikuwa amri ambayo kwa maneno mengine ikaitwa jihadi. Na ibara yenyewe ya amri hii imo ndani ya Kurani Tukufu mpaka sasa ambayo ndiyo hii:

أُذِنَ لِلَّذِيْنَ يُقٰتَلُوْنَ بِاَنَّهُمْ ظُلِمُوْا ؕ وَاِنَّ اللّٰهَ عَلٰى
نَصْرِهِمْ لَقَدِيْرُ ۙ﴿۳۹﴾ الَّذِيْنَ اُخْرِجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ[3]

Yaani, Mungu Amesikia kilio cha hao waliodhulumiwa ambao wanauawa na wakafukuzwa majumbani mwao pasipo haki, na wakaruhusiwa kushindana, na Mungu Anaweza kumsaidia aliyedhulumiwa (Juzu 17, surat-ul-Haj). Lakini amri hii ilikuwa kwa zama na muda maalum, si kwa kudumu, bali ilihusu zama zile ambapo wenye kusilimu walikuwa wakichinjwa kama mbuzi na kondoo. Lakini ni masikitiko kwamba baada ya zama za unabii na ukhalifa watu wakaangukia makosa mkubwa sana katika kuelewa swala la jihadi ambalo msingi wake ndio aya takatifu iliyotajwa hapo juu, na ikafikiriwa kwamba ni desturi ya kidini kuwachinja kwa panga viumbe wa Mungu pasipo haki. Na jambo la ajabu ni kwamba Wakristo walikosea kuhusu haki za Muumba, na Waislamu kuhusu haki za viumbe. Yaani, katika dini ya Kikristo kwa kumfanya mtu mnyonge kuwa Mungu, akanyanganywa haki Mungu Mweza na Mhifadhi wa milele, ambaye hakuna kilichofanana naye

[3] Al-Hajj, 22:40-41

ardhini wala mbinguni; na Waislamu wakanyang'anya haki za wanadamu kwa kutumia upanga pasipo haki na wakaiita jihadi. Ilmuradi njia moja ya kunyang'anya haki wakaishika Wakristo, na njia nyingine ya kunyang'anya haki wakaishika Waislamu. Na kwa bahati mbaya ya zama hizi makundi haya mawili yanazifikiria namna zote mbili za kunyang'anya haki kuwa njia ya kupendeza, na kila kundi ambalo linaikazania sawa na itikadi yake namna mojawapo ya unyang'anyi wa haki linadhani litakwenda peponi moja kwa moja kwa sababu hiyo, wala hamna njia bora zaidi ya kwenda Peponi kuliko hiyo. Na ingawa dhambi ya kumnyang'anya Mungu haki yake ni dhambi kubwa kuliko dhambi zote, lakini hapa kusudio letu si tutaje huu unyang'anyi wa hatari wa haki unaotendwa na taifa la Kikristo, bali tunataka hapa kuwatanabahisha Waislamu kuhusu unyang'anyi wao wa haki ya wanadamu.

Ikumbukwe kwamba maulamaa wa Kiislamu wa siku hizi wanaoitwa Maulawii wanavyoelewa masiala ya jihadi na jinsi wanavyoeleza swala hili mbele ya umma, siyo sahihi kabisa. Na matokeo yake ndiyo haya tu kwamba watu hao kwa mawaidha yao yenye kusisimua wawafanye watu wa kawaida wenye taibia ya kinyama kuwa katili

na kuwaondolea sifa zote tukufu za kibinadamu. Na ikawa vivyo hivyo. Nami najua kwa yakini kwamba wote waliouliwa pasipo haki na hao watu wajinga na wenye kufuata tamaa za nafsi zao wasioielewa siri hii kwamba kwa nini na kwa sababu gani Islam katika zama za mwanzo wake ilihitajika kupigana vita, dhambi za hao wote ndiyo juu ya hao Maulawii ambao wanaendelea kufundisha masiala ya aina hii kwa siri, ambayo yanasababisha mauaji ya kutia uchungu. Hao watu wanapokutana na watawala wanainama kiasi hiki kuwaamkia kana kwamba wako tayari kusujudu; na wanapoketi katika vikao vya wenzao basi hukazania mara kwa mara kwamba nchi hii ndiyo zoni ya vita, na mioyoni mwao wanaamini kwamba kupigana jihadi ni faradhi. Na ni wachache tu wasio na fikara hii. Watu hawa wameshika sana itikadi ya jihadi iliyo batili kabisa na kinyume cha Kurani na Hadithi, kiasi hiki kwamba mtu ambaye hana itikadi hii na anaipinga wanamwita dajali na kumtolea fatuwa kwamba auawe. Mimi nami niko chini ya fatuwa hii tangu muda mrefu. Na baadhi ya masheikh wa nchi hii wameniita dajali na kafiri. Na bila kujali sheria ya serekali ya Kiingereza wakaeneza dhidi yangu fatuwa iliyochapishwa kwamba mtu huyu anawajibika auawe, na kunyang'anya mali yake

bali kuwateka wanawake ni jambo la thawabu kubwa. Sababu yake ilikuwa nini? Sababu ya hasira yao na uadui wao ikawa kuwa kwangu Masihi Mau‘udi na kutoa mawaidha kinyume cha masiala yao ya kijihadi na kubatilisha kabisa ujaji wa Masihi mwaga damu na Mahdi mwaga damu ambaye katika ujaji wake waliweka matumaini makubwa makubwa ya kunyang‘anya na kuteka mali ya watu. Lakini wazingatie kwamba kwa kweli hakika ya jihadi kama wafikirivyo mioyoni mwao si sahihi, na hatua yake ya kwanza ndiyo kufutilia mbali huruma ya kibinadamu. Fikara yao hii si sawa katu kwamba ikiwa katika zama za mwanzo wa Islam jihadi ilikuwa sawa, kwa nini iwe haramu sasa? Tunayo majibu yake mawili: La kwanza ni kwamba wazo hili ni kukisia visivyo, Mtume wetu s.a.w. hakutumia kabisa upanga dhidi ya mtu yeyote isipokuwa wale ambao walitangulia kutumia upanga na wakawaua bila kuona huruma wanaume na wanawake wema wasiokuwa na hatia, na watoto. Na wakawaua kikatili sana hata kwamba leo pia mtu aanza kulia kwa kuzisoma habari hizo. La pili, hata kama tukikubali kwamba katika Islamu ilikuwepo ile jihadi wanavyofikiria masheikh, hata hivyo katika zama hizi amri ile haipo tena, kwani imeandikwa kwamba Masihi Mau‘udi atakapodhihiri, jihadi ya

upanga na vita vya kidini vitakoma. Maana, Masihi hatainua upanga wala hatashika mkononi silaha nyingine yoyote ya kiardhi, bali dua yake itakuwa silaha yake, na nia yake thabiti itakuwa upanga wake. Ataweke msingi wa suluhu na atawafanya wanyonge na wenye nguvu wakae pamoja kwa amani. Na zama zake zitakuwa zama za suluhu, upole na huruma ya kibinadamu. Ole wao! Kwa nini hao watu hawazingatii kwamba miaka elfu moja na mia tatu imepita tangu Mtume Mtukufu s.a.w. alipotamka kuhusu Masihi aliyeahidiwa maneno يضع الحرب[4] ambayo maana yake ni kwamba Masihi Mau'udi atakapokuja atamaliza vita, na kwenye habari hiyo aya hii ya Kurani inaashiria:

حَتّٰى تَضَعَ الْحَرْبُ اَوْزَارَهَا ۛ[5]

Muradi wake, mpigane mpaka ziwadie zama za Masihi. Hiyo ndiyo maana ya: تضع الحرب اوزارها

Angalieni! Sahihi Bukhari kipo kilichokubaliwa kuwa sahihi kuliko vitabu vyote baada ya Kurani Tukufu. Kisomeni kwa makini. Enyi maulamaa na masheikh wa Islam! Nisikilizeni! Nasema kweli kabisa kwamba huu sio wakati wa jihadi;

---

[4] Sahihi Bukhari, Kitabul Ambiya, Bab Nuzuli Isa

[5] Sura Muhammad, 47:5

msimwasi Mtume Mtukufu wa Mungu. Masihi Mau‘udi aliyekuwa aje amekwisha fika tayari, na kaamuru pia kwamba sasa epukaneni na vitu vya kidini vinavyopiganwa kwa upanga na vinasababisha mauaji na umwagaji wa damu. Kama bado hamwachi umwagaji wa damu na hamfumbi midomo yenu kutoa mawaidha ya aina hiyo, basi hiyo siyo njia ya Islamu. Yule aliyenikubali huyo si tu atafumba midomo yake asitoe mawaidha ya namna hii, bali na ataitambua njia hii kuwa ni mbaya sana na ni yenye kusababisha ghadhabu ya Mungu.

Hapa tunalazimika kuandika pia kwa kusikitika kwamba kama vile upande mmoja masheikh majahili walivyowafundisha watu wa kawaida hila za kunyang’aya mali za watu na kuwaua binadamu na wakaiita jihadi kwa kuficha hakika yenyewe ya jihadi, ndivyo hivyo upande wa pili walivyofanya mapadri pia na wakichapisha maelfu ya vijitabu na matangazo katika lugha za Kiurdu, Kipashto na kadhalika wakaeneza katika India, Panjab na nchi zinazopakana na nchi hii kwamba Islamu ilienea kwa upanga na Islam ndiyo kutumia upanga. Matokeo yake ni kwamba watu wa kawaida kwa kupata shuhuda mbili za jihadi — maanake, kwanza ushuhuda wa

masheikh na wa pili ushuhuda wa mapadri — wakaongezeka harara ya ukatili wao. Nionavyo mimi, yailazimu serekali yetu mhisani iwazuie hawa mapadri wasizue uzushi huu wa hatari ambao matokeo yake ni uchafuzi wa amani na uasi nchini. Hii haiyumkiniki kwamba kwa uzushi huo mbovu wa mapadre, Waislamu wataacha dini ya Kiislam; naam, matokeo ya mahubiri hayo daima yatakuwa tu kwamba watu wa kawaida wataendelea kukumbushwa habari ya jihadi na watazinduka usingizini. Ilmuradi, sasa Masihi Mau'udi alipokwishafika, ni faradhi ya kila Mwislamu aachane na jihadi. Kama nisingalikuwa nimekuja, pengine kungalikuwa na udhuru kidogo wa kosa la kutokufahamu; lakini nimekwishafika sasa, nanyi mmeshaona siku ya ahadi. Kwa hiyo, watumiaji wa upanga kidini sasa hawana udhuru wowote mbele ya Mwenyezi Mungu. Yule aliye na macho na anazisoma hadithi na kuitalii Kurani, anaweza kufahamu vizuri kwamba njia hii ya jihadi waliyoishikilia katili wengi wa zama hizi, siyo jihadi ya Kiislamu; bali haya ni matendo yasiyojuzu yaliyoenea baina ya Waislamu, yaliyosababishwa na jazba za nafsi inayoamrisha kutenda maovu au tamaa ya bure ya kwenda Peponi. Mimi nimeshaeleza sasa hivi kwamba Mtume wetu s.a.w. katika zama zake hakutangulia

kabisa kuinua upanga, bali kwa muda mrefu alisumbuliwa kwa mkono wa makafiri na akaonyesha subira asiyoweza kila mtu. Na kadhalika masahaba zake nao wakashikamana na kanuni hiyo njema. Na jinsi walivyoamriwa kusumbuka na kusubiri, ndivyo walivyoonyesha ikhlasi na subira. Wakakanyagwa chini ya miguu, lakini hawakulalamika. Watoto wao walikatwa vipande vipande mbele yao, wakaadhibiwa kwa moto na maji; lakini wakajizuia wasishindane na shari kana kwamba ndio watoto wachanga. Nani awezaye kuthibitisha kwamba duniani kuna umati mmojawapo kati ya nyimati za manabii wote ambao baada ya kusikia amri ya Mungu ulijifanya mnyonge na kuachana na kushindana na maadui juu ya kuwa na uwezo wa kijilipiza kisasi, jinsi walivyojifanya hao? Nani anao uthibitisho wa jambo hili kwamba katika dunia kulikuwa na kundi lolote lingine ambalo juu ya kuwa na ushujaa, jumuiya, nguvu, uwezo wa kushindana, na kuwa na sifa za utu ume na ushujaa, likaendelea kusubiri kwa miaka kumi na mitatu juu ya kuudhiwa na kujeruhiwa na maadui katili? Subira hii ya Sayyidi na Bwana wetu na masahaba zake haikuwa kuwa udhaifu, bali katika zama hizo za subira pia masahaba wajitoleao walikuwa na mikono hiyo hiyo walivyoitumia baada ya

kuamrishwa kufanya jihadi. Na wakati mwingine vijana elfu moja waliwashinda maaskari wapiganaji laki moja wa wapinzani. Ikawa hivi ili watu wajue kwamba subira waliyoonyesha katika Makka juu ya ukatili wa maadui haikuwa kwa sababu woga na unyonge, bali kwa kusikia amri ya Mungu wakaacha silaha na wakawa tayari kuchinjwa kama mbuzi na kandoo. Bila shaka subira ya aina hii yazidi uwezo wa kibinadamu. Na tukisoma historia ya dunia nzima na ya manabii wote, hatukuti khulka njema hizo katika umati wowote na katika wafuasi na nabii yeyote. Na kama tunasikia habari ya subira ya baadhi ya watu wa zamani, mara inapita moyoni kwamba dalili inaonyesha uwezekano wa subira hiyo kwa kweli iwe kwa sababu ya woga na kukosa uwezo wa kulipiza kisasi. Lakini kundi la watu ambao kwa kweli wanao ufundi wa kiaskari na ni mashujaa na wenye moyo madhubuti, kisha wateswe na watoto wao wauawe na wajuruhiwe kwa kupigwa mikuki, lakini hata hivyo wasishindane na uovu, hii ndiyo sifa ile ya utu ume ambayo ilidhihirishwa kikamilifu yaani kwa miaka kumi na mitatu mfululizo na Mtume wetu Mtukufu na masahaba zake. Subira ya aina hii ambapo kila saa walikabili mabalaa yaliyoendelea hadi muda wa miaka kumi na mitatu, kwa kweli

haina kifani; na kama mtu ana shaka, basi na atuambie kwamba mfano wa subira ya aina hii uko wapi katika wakweli wa zamani?

Na hapa jambo hili pia lapaswa kukumbuka kwamba dhuluma nyingi kiasi hicho waliyofanyiwa masahaba, wakati wa dhuluma ya namna hiyo Mtume wetu s.a.w. hakuwaambia njia yoyote ya kujilinda kwa kufikiria mwenyewe, bali mara kwa mara akasema tu subirini juu ya mateso hayo yote. Na kama mtu aliomba ruhusa ya kushindana nao, basi akamzuia akisema nimeamriwa kufanya subira. Ilmuradi, daima Mtume Mtukufu s.a.w. aliendelea kusisitizia subira mpaka amri ya kushindana ikaja kutoka mbinguni. Sasa tafuteni mfano wa subira ya aina hii katika watu wote wa awali na wa baadaye. Kisha kama iyumkinike, tafuteni mfano wake katika wafuasi wa Hadhrat Musa au katika wanafunzi wa Hadhrat Isa a.s. kisha tuelezeni.

Muhtasari wa mazungumzo ni kwamba iwapo Waislamu wanao mfano huu wa subira na kujiepusha na shari na hulka njema, ambao wanaona fahari kwayo mbele ya dunia nzima, basi ni ujinga gani huu na bahati mbaya na nuhusi ya amali kwamba mfano huu sasa umetupiliwa mbali! Masheikh majahili — Mungu Awape

mwongozo — wamewadanganya sana watu wa kawaida. Na wamesema ufunguo wa kuingia Peponi ndio kitendo hicho hicho kilicho dhuluma dhahiri na ukatili na kinyume na hulka ya kibinadamu. Je, hii inaweza kuwa kitendo chema kwamba mtu fulani, kwa mfano, kwa mawazo yake anaenda madukani, nasi hatuhusiani naye kabisa, hata hatujui jina lake wala huyo hatujui, lakini kwa kumwua tumemfyatulia risasi. Je, hii ndiyo maana ya dini? Kama hicho ni kitendo chema, basi wanyama mbuai wanawazidi binadamu katika wema wa aina hii! Mungu Atukuzwe! Watu hao walikuwa wakweli namna gani na walikuwa na roho ya manabii ndani mwao, maana Mungu alipowaamuru huko Makka kwamba msishindane na uovu hata mkikatwa vipande vipande, basi wakawa wanyonge na wadhaifu kama watoto wachanga baada ya kupata amri hii, kana kwamba mikono yao imeishiwa nguvu. Baadhi yao wakauawa kwa njia hii pia kwamba ngamia wawili wakasimamishwa pamoja, na miguu yao (hao waumini) ikafungwa kikiki kwa ngamia hao kisha ngamia wakakimbizwa kuelekea pande tofauti, nao wakachanika papo hapo inavyokatwa karoti au figili. Lakini ni masikitiko kwamba Waislamu na hususan masheikh hawajali matukio hayo yote. Na

sasa wanadhani kana kwamba dunia nzima ndiyo windo lao. Na kama vile mwindaji baada ya kumgundua swala katika pori fulani, anamwendea kwa kujificha-ficha na hatimaye kwa kupata fursa anafyatua bunduki, hivyo ndivyo zilivyo hali za masheikh wengi. Hawajui katu huruma ya kibinadamu ni kitu gani; kwao kumfyatulia bila sababu bastola au bunduki mtu asiyetazamia imefahamika kuwa ndiyo Islamu. Wako wapi kati yao ambao wapate kupigwa na wakasubiri. Je, Mungu Ametuamrisha kwamba sisi bila sababu yoyote pasipo uthibitisho wa hatia yoyote tumdunge mtu kisu na kumkata vipande vipande au tumwue kwa bunduki kwa kumkuta hayuko macho, ilhali hatumjui yeye wala hatujui sisi. Je, dini ya aina hii yaweza iwe imetoka kwa Mungu inayofundisha mwendelee kuwaua watu wa Mungu wasio na dhambi, wasio na hatia, wala hawajahubiriwa nanyi mtaingia Peponi! Ni jambo la kusikitisha, tena ni la aibu, kwamba mtu ambaye hatuna uadui naye wowote wa zamani, bali hata hatumtubmui, yeye anawanunulia watoto wake kitu kutoka duka fulani au ameshughulikia kazi yake halali, nasi bila sababu yoyote pasipo uhusiano wowote tukamfyatulia bunduki na kumfanya mara moja mke wake kuwa mjane, watoto wake kuwa mayatima na nyumba yake

kuwa penye maombolezo. Njia hiyo imeandikwa katika Hadithi gani au imeandikwa katika aya gani? Yuko sheikh yeyote aijibuye? Majahili wamesikia neno 'jihadi', kisha kwa udhuru huu wametaka kutimiza tamaa za nafsi zao, ama kwa wazimu tu wamepata kumwaga damu. Tumeshaandika sasa hivi kwamba katika zama za Mtume wetu s.a.w. Islam ilipoinua upanga, huo ukainuliwa ambapo Waislamu wengi walikwisha ingia makaburini kwa panga za makafiri. Hatimaye ghera ya Mungu ikataka kwamba watu wauao kwa panga nao wauawe kwa panga. Mungu ndiye Karimu, Rahimu na Mpole na mwenye kuvumilia sana, lakini hatimaye Yu Mwenye ghera pia kwa wakweli. Nastaajabia kwamba mtu yoyote asipowaua Waislamu katika zama hizi kwa sababu ya dini, basi kwa amri gani hao wanawaua watu wasio na hatia. Kwa nini masheikh wao hawawakatazi kufanya matendo hayo yasiyofaa yanayovunja sifa ya Islamu. Chini ya serekali hii ya Kiingereza, Waislamu wanapata raha nyingi namna gani; je yupo yeyote awezaye kuzihesabu? Bado wengi watakuwa hai walioshuhudia kadiri fulani zama za Makalasinga. Sasa hao hao waelezee katika zama za Makalasinga ilikuwaje hali ya Waislamu na Islamu. Desturi moja ya muhimu ya Islamu ya

kutoa adhana ya sala ilichukuliwa kuwa hatia. Kulikuwa hakuna ambaye angethubutu kutoa adhana kwa kupaza sauti kisha angeepuka mafumo na mikuki ya Makalasinga. Basi sasa, je, Mungu Amefanya vibaya kwamba Akawaokoa Waislamu katika dhuluma ya Makalasinga na kuwajalia utawala wa amani wa serekali ya Kiingereza. Na kwa ujaji wa serekali hii Waislamu wa Panjab kana kwamba wakasilimu upya. Kwa kuwa malipo ya hisani ndiyo hisani, kwa hiyo haitupasi tukatalie neema hii ya Mungu, tuliyojaliwa baada ya maelfu ya maombi, badala ya utawala wa Makalasinga.

Nami wakati huu nawasihi kwa kukazania jumuiya yangu wanaoniamini kuwa Masihi Mau‘udi kwamba waachane na mazoea haya mabovu. Mungu Amenituma nikiwa Masihi Mau‘udi na Amenivika vazi la Hadhrat Masihi bin Mariamu, kwa hiyo nasihi kwamba mwepukane na shari na mwahurumie wanadamu. Mwitakase mioyo yenu isiwe na bughudha na inadi kwani kwa mazoea haya mtakuwa kama malaika. Chafu na najisi ilioje dini ile ambamo hamna huruma kwa binadamu, na najisi ilioje njia ile iliyojaa miba ya bughudha ya nafsi. Basi nyinyi mlio pamoja nami msiwe hivyo. Fikirini mmefaidika

nini na dini. Je, hii tu kwamba saa zote mazoea yenu yawe kuwaudhi watu? Hasha, bali dini ndiyo kwa kupata maisha yale yaliyomo ndani ya Mungu. Na maisha hayo hakuyapata mtu wala hatayapata hata baadaye isipokuwa hapo tu ambapo sifa za Mungu ziingie ndani ya mtu. Kwa ajili ya Mungu warehemuni wote ili mrehemiwe kutoka mbinguni. Njoni, nikawafundishe njia itakayoifanya nuru yenu izishinde nuru zote, nayo ndiyo hii kwamba mwachane na inadi na husuda zote mbovu na muwe mnawahurumia wanadamu na mjipoteza ndani ya Mungu. Na pamoja na hayo mjipatie utakaso wa hali ya juu. Hiyo ndiyo njia ambayo kwayo miujiza inatendeka na maombi yanakubalika na malaika wanashuka kusaidia. Lakini hii siyo kazi ya siku moja; jisogezeeni mbele, jisogezeeni mbele. Jifunzeni kwa dobi yule ambaye kwanza anazichemsha nguo katika marigedi na anazidi kuchemsha mpaka athari za moto zinatenga uchafu na taka za aina zote kutoka kwa nguo. Kisha anaamka asubuhi na anafika penye maji na analowesha nguo katika maji na anazipiga-piga mara kwa mara juu ya mawe, ndipo uchafu ule uliokuwa ndani ya nguo na ukawa sehemu yake, mara moja unaanza kutengana, kidogo kwa kuchemshwa katika maji ya moto na kidogo kwa kupigwa-pigwa na mkono

wa dobi kwa kuzilowesha katika maji, mpaka nguo zinakuwa nyeupe kama zilivyokuwa mwanzoni. Hiyo ndiyo njia ya kuwa nyeupe kwa nafsi ya binadamu, na wokovu wenu wote unautegemea weupe huu. Hilo ndilo jambo ambalo Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurnai Tukufu:

قَدۡ اَفۡلَحَ مَنۡ زَكّٰىهَا ۝١٠ [6]

Yaani, nafsi ile imepata kuokoka iliyotakaswa katika uchafu wa aina aina. Angalieni! nimewajieni nikileta amri moja nayo ndiyo kwamba sasa jihadi ya upanga imekwisha, lakini jihadi ya kujitakasa nafsi zenu inaendelea. Na sikulisema hilo kwangu binafsi, bali hilo ndilo kusudio la Mungu. Kumbukeni Hadithi ile ya Sahihi Bukhari ambapo imeandikwa kumhusu Masihi Mau'udi kwamba يضع الحرب

Yaani, Masihi atakapofika, atamaliza vita vya kidini. Basi nawaamrisha walioingia katika jeshi langu waondokewe na mawazo hayo. Wajitakase mioyo yao na wakuze huruma yao ya kibinadamu na wawahurumie wenye matatizo. Waeneze suluhu ardhini, kwani kwa njia hiyo dini yao itaenea. Na wasistaajabie kwamba itakuwaje

---

[6] Ash-Shams, 91:10

hivyo! Kwani, kama vile Mungu pasipo kupitia njia za kawaida Alivyotumia kwa mahitaji ya kimwili katika uvumbuzi mpya wa zama hizi, elementi za ardhi na vitu vyote vya ardhini, na Akakimbiza magarimoshi kwa kupita hata mafarasi pia, ndivyo Yeye Atakavyotumia sasa malaika wa mbinguni kwa mahitaji ya kiroho bila kupitia mikono ya kibinadamu. Ishara kubwa kubwa za kimbinguni zitadhihirika, na ming'ao mingi itazuka itakayofumbua macho ya wengi, ndipo mwishoni watu wataelewa kwamba minghairi ya Mungu watu na vitu vingine vilivyofanywa kuwa Mungu, hayo yote yalikuwa makosa. Basi mwendelee kusubiri kwani Mungu anayo ghera zaidi kuliko nyinyi kwa ajili ya tauhidi yake. Na mwendelee kushughulikia kuomba isije mkaandikwa katika waasi. Enyi wenye njaa na kiu ya ukweli, sikilizeni kwamba hizi ni siku ambazo ziliahidiwa tangu mwanzo. Mungu hataahirisha sana mambo haya. Na jinsi mnavyoona kwamba taa inapowekwa juu ya mnara mrefu, basi mwanga wake unaenea mpaka mbali sana, au umeme unapometa upande mmoja mbinguni, pande zote zamulikika, ndivyo itakavyokuwa siku hizi. Kwani, Mungu kwa kutimiza bishara yake kwamba mahubiri ya Masihi yatatapakaa duniani kama umeme, au

kama mwanga wa taa ya mnara mrefu yataenea katika pande nne za dunia Ameisha andaa kila njia ardhini, na ameanzisha kikamilifu mipango mizuri ya garimosi, telegramu, meli na posta na njia rahisi za utalii. Basi hivyo vyote vilifanywa vipatikane ili itimie habari hii kwamba mwito wa Masihi Mau‘udi utang’arisha kila kona kama umeme. Na mnara wa Masihi uliotajwa katika Hadithi, kwa kweli uhakika wake ni huu tu kwamba mwito na nuru ya Masihi utaenea duniani haraka sana jinsi kutoka mnara mrefu sauti na nuru inavyofika mbali sana. Hivyo, garimoshi, telegramu, meli, posta na njia zote za kurahisisha mahubiri na kurahisisha safari ni alama maalum ya zama za Masihi ambayo manabii wengi wameitaja. Na Kurani pia inasema:

وَاِذَا الۡعِشَارُ عُطِّلَتۡ ۪ۙ[7]

Yaani, zama za mwito kwa wote zilizo zama za Masihi Mau‘udi[8] ndizo zama ambapo ngamia

---

[7]At-Takwiir, 81:5

[8]Nimeshaandika mara kwa mara kwamba Masihi Mau‘udi siye nabii wa Kiisraeli bali amekuja akipata tabia na silika zake. KatikaTorati, Mtume wetu s.a.w. amefananishwa na Musa, basi ilibidi kwamba sawa na silisila ya Musa, mwishoni mwa silisila ya Muhammad s.a.w. pia Masihi mmoja awepo. Mwandishi.

hawatafaa, yaani njia mpya ya usafiri itapatikana kwa hiyo ngamia hawatahitajika. Na katika Hadithi pia imo kwamba: يترك القلاص فلا يسعٰى عليها

Yaani, katika zama zile ngamia hawatafaa. Na zama za nabii mwingine yeyote hazikuwekewa alama hii. Basi, shukuruni kwamba yanafanywa matayarisho huko mbinguni kwa kueneza nuru. Katika ardhi zinataharaki baraka za ardhi, yaani, safarini na nyumbani na katika kila jambo mnashuhudia raha ambazo mababu zenu hawakuziona, kana kwamba dunia imegeuka kuwa mpya. Matunda yanaweza kupatikana katika wakati mmoja pasipokuwa msimu wake. Safari ya miezi sita inaweza kuwa katika siku chache. Habari kutoka maelfu ya maili zinaweza kufika mara moja. Kwa kurahisisha kila kazi mashine na mitambo inapatikana. Kama mkitaka mnaweza kusafiri katika garimoshi kama mlivyo katika bustani ya nyumbani. Je, hayajatokea mapinduzi ardhini? Basi, kwa kuwa mapinduzi ya ajabu yametokea ardhini, hivyo, Mungu Mweza Anataka hata mbinguni pia mapinduzi ya ajabu yatokee. Na hizo zote mbili ndizo alama za zama za Masihi. Na kuna ishara kwenye alama hizo hizo zilizomo katika ufunuo mmoja uliomo katika kitabu changu *'Barahin-e-Ahmadiyya'*,

ulioandikwa miaka ishirini kabla. Nao ndio huu:

اَنَّ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضَ كَانَتَا رَتۡقًا فَفَتَقۡنٰهُمَا[9]

Yaani, ardhi na mbingu zote mbili zilikuwa zikifungwa kama mzigo, ambazo sifa zao zilifichikana. Nasi katika zama za Masihi tuliifungua mizigo yote miwili na kudhihirisha sifa za hiyo miwili.[10]

Mwishoni ikumbukwe kwamba ingawa tumeshaandika kwa kirefu katika kijitabu hiki kwamba njia hii iliyopo ya kuwashambulia wafuasi wa dini nyingine, ipatikanayo baina ya Waislamu wanayoiita jihadi, hii siyo jihadi ya kisheria, bali ni kinyume kabisa cha amri ya Mungu na Mtume s.a.w. na ni dhambi kubwa, lakini kwa vile baadhi ya makabila ya Kiislamu yamekwisha zoea kushikilia njia hii, kwa hiyo haiyumkiniki kwao kwa urahisi kuachana na mazoea haya; bali yumkini wawe maadui katili wa

---

[9]Al-Anbiyaa, 21:31

[10]Je si kweli kwamba katika zama hizi mzigo wa ardhi umefunguka namna ambavyo kwamba maelfu ya mambo mapya ya hakika, sifa na mitambo inaendelea kudhihirika. Kwa nini, basi mzigo wa mbingu ubaki ukifungika. Kuhusu mzigo wa mbingu, manabii wa zamani nao walitabiri kwamba watoto na wanawake pia watafunuliwa na Mungu, na hizo zitakuwa zama za Masihi Mau‘udi. Mwandishi.

yule awasihiye na kwa jazba ya kighazi wanuie kumwua. Naam, ipo njia moja ninayofikiria moyoni mwangu, nayo ni hii kwamba kama Bwana Amiri, mfalme wa Kabul, anayeheshimika katika makabila ya Maafghan kiasi hiki kwamba labda mfano wake hautapatikana katika Amiri yeyote wa Kiafghani wa zamani, kama akiwakutanisha maulamaa mashuhuri, alifanye swala hili la jihadi lijadiliwe, kisha kwa njia ya maulamaa awatanabahishe watu wa kawaida kuhusu makosa yao, bali akiandikisha vijitabu vichache katika lugha ya Kipashto na maulamaa wa nchi hiyo, avisambaze kwa vingi, basi, kwa yakini juhudi ya namna hii itawaathiri sana watu, na harara ile wanayotapakaza masheikh wajinga baina ya watu wa kawaida itapungua pole pole. Na kwa yakini itakuwa bahati mbaya ya raia wa Amiri ikiwa Amiri hatajali marekebisho haya ya muhimu. Na matokeo yake ya mwisho ndiyo matatizo kwa serekali hiyo inayonyamaza juu ya fatuwa za namna hii za masheikh. Kwani, siku hizi masheikh na maulamaa hao wanayo mazoea kwamba wanamkufurisha mtu au dhehebu fulani kwa hitilafu kidogo ya kidini kisha zile fatuwa zao za jihadi na kadhalika zilizopo kuhusu makafiri wanazijirisha dhidi ya hao pia. Basi, katika hali hii Amiri pia hawezi kusalimika na fatuwa hizo.

Yumkini hao masheikh wakati mwingine wakimkasirikia Amiri kwa jambo dogo wamtoe nje kutoka katika dini ya Kiislamu, kisha kwa fatuwa zile zile za jihadi ziandikwe dhidi yake pia ambazo wanawaandikia makafiri. Basi, bila shaka, watu ambao wanayo madaraka ya kumfanya mtu kuwa mumini au kafiri na kisha kumwandikia fatuwa ya jihadi dhidi yake, ni watu wa hatari ambao Amiri pia asitulie kwa upande wao. Na bila shaka watu hao ndio chanzo cha uasi kwa kila serikali. Raia maskini wako chini ya mamlaka ya watu hao, na mioyo yao imo katika mkono wao, waielekeze upande wowote wautakao na papo hapo waulete uharibu mkubwa. Basi, si jambo la dhambi kwamba raia watolewe katika kucha zao, na kwa upole wafahamishwe hakika yenyewe ya swala la jihadi. Islamu haifundishi kamwe kwamba Waislamu wawe kama maharamia na wezi na watimize tamaa za nafsi yao kwa udhuru wa kufanya jihadi. Na kwa kuwa katika Islamu jihadi haisihi katu bila amri ya mfalme, na raia pia wanaijua, hivyo, inahofiwa kwamba watu wasio na habari ya uhakika ulivyo, wamlaumu mfalme mioyoni mwao kwamba kwa idhini yake hayo yote yanatendeka. Kwa hiyo, hii ni faradhi kabisa ya Amiri kujibidiisha sana iwezekanavyo kukomesha fatuwa hii potofu, kwani hapo

itaonekana kama jua ling'aavyo kwamba Bwana Amiri hahusiki na habari hii na thawabu pia ataipata. Kwani, kwa kuangalia haki za wanadamu hakuna wema zaidi kuliko kuokoa shingo za waliodhulumiwa katika panga za wadhalimu. Na kwa kuwa wafanyao matendo kama hayo, na kutumia upanga kwa nia ya kuwa ghazi, wengi wao ndio Maafghan ambao wengi wao wanaishi katika nchi ya Amiri, kwa hiyo Mwenyezi Mungu Amemjalia Amiri nafasi hii kwamba katika kazi zake kubwa za uamiri wake aache nyuma yake kumbukumbu la urekebisho huu adhimu. Na mazoea hayo ya kikatili yanayoharibu jina la Uislamu, awaachishe Waafghani hayo sawa na uwezo wake. La, sivyo, sasa zama za Masihi Mau'udi zimeshawadia; sasa kwa vyovyote Mwenyezi Mungu Ataleta sababu kutoka mbinguni hata kwamba ardhi iliyojaa dhuluma na umwagaji wa damu bila haki, sasa itajaa uadilifu, amani na usuluhisho. Na watabarikiwa wale maamiri na wafalme ambao watashughulikia kiasi chochote kutekeleza jambo hili.

Baada ya kuandika hayo yote, ningependa kuieleza serekali yetu mhisani habari moja. Ingawa najua serekali yetu hii ni serekali yenye akili na busara, lakini ni faradhi yetu pia kwamba kama kuna shauri yoyote njema iifaayo serekali na

watu wote kwa jumla, basi na tuitoe. Nayo ndiyo hii kwamba nionavyo mimi, ni jambo la hakika na la yakini kwamba mazoea hayo ya kikatili yanayopatikana katika Waafghan wa mpakani na mara kwa mara mtu asiye hatia anauawa, sababu zake nilivyokwishaeleza ni mbili; (1) kwanza wale masheikh ambao wanayo itikadi kwamba kuwaua watu wa dini zingine na hasa Wakristo ni jambo la thawabu kubwa na kwa njia hii neema kubwa sana za Peponi zitapatikana ambazo haziwezi kupatikana kwa sala wala hija wala zaka wala kwa kitendo kingine chochote chema. Naelewa vizuri kwamba watu hao wanaendelea kisirisiri kuwafikishia watu wa kawaida mawaidha kama hayo. Hatimaye kwa kusikia usiku na mchana mawaidha kama hayo, watu hao ambao baina yao na hayawani kuna tofauti kidogo tu, wanaathirika sana na wanakuwa wanyama mbuai na hawabakiwi na huruma hata kidogo na wanamwaga damu kikatili hata kwamba mwili unatetemeka. Na ingawa nchi za mipakani na za Kiafghani zimejaa sana masheikh wa aina hii ambao wanatoa mawaidha kama hayo, lakini rai yangu ndiyo kwamba katika Panjab na India pia masheikh wa aina hii hawakosekani. Kama serekali tukufu imeyakinia kwamba masheikh wote wa nchi hii hawana kabisa mawazo kama hayo, basi yakini hiyo bila shaka inapaswa

kufikiriwa upya. Nionavyo, masheikh wengi wanaokaa msikitini wasioelimika, wepesi wa kuhamaki, ndio ambao hawajaepukana na mawazo hayo machafu. Kama wangekuwa na mawazo kama hayo sawa na mwongozo wa Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu, hapo ningewachukulia wenye udhuru, kwani kwa kweli mtu huwa na udhuru katika mambo ya itikadi. Lakini nasema kweli kabisa kwamba hao kama walivyo maadui wa kisirisiri wa serekali hii adilifu kusahau hisani za serekali, ndivyo walivyo wenye hatia na waasi wa Mwenyezi Mungu. Kwani nimekwisha eleza kwa kirefu kwamba Neno la Mwenyezi Mungu halifundishi kabisa tuwaue hivyo wasiokuwa na hatia, na aliyeelewa hivi anatengana na Islamu. (2) Sababu ya pili ya mauaji hayo ya kihalifu yanayofanyika kwa udhuru wa kuwa ghazi, katika rai yangu, ndio mapadre pia waliosisitiza kupita kiasi kwamba katika Islamu jihadi ni faradhi, na kuua mataifa mengine ni jambo la thawabu kubwa katika dini ya Waislamu. Nionavyo mimi, watu wa mpakani hata hawakuwa na habari ya swala la jihadi. Hilo wamelikumbusha mapadre. Ninayo dalili hii kuthibitisha fikara yangu kwamba matukio kidogo sana kama hayo yalikuwa yanasikika bali twaweza kusema kulikuwa hakuna kabisa kabla mapadre walikuwa hawajaeneza magazeti,

majarida na vitabu kama hivyo katika nchi za mpakani. Bali, serekali ya Makalasinga ilipokwisha nchini humu na mahali pao wakaja Waingereza hapo Waislamu kwa jumla wakafurahi sana kwa mapinduzi hayo, na watu wa mpakani pia wakafurahi mno. Kisha mnamo mwaka 1849 Padre Pfander alipoandika kitabu "*Mizan ul Hak*" na kutapakaza katika India, Panjab na nchi za mpakani, na humo si tu alitumia maneno ya kuondolea heshima Islamu na Mtume wa Islamu s.a.w., bali akaeneza baina ya malaki ya watu kwamba katika Islamu kuwaua wafuasi wa dini zingine si tu inaruhusiwa, bali ni thawabu kubwa. Kwa kusikia maneno haya hayawani wa mpakani wasioelewa chochote cha dini yao wakaamka na wakawa na yakini kwamba bila shaka katika dini yetu kuwaua wafuasi wa dini zingine ni jambo la thawabu kubwa. Nimetafakari kwa makini sana kwamba matukio mengi ya mpakani na uadui mkali unaopatikana katika watu wa mpakani sababu yake ndiyo vitabu vya mapadre walimopita kiasi hao kutumia maneno makali na kueleza mara kwa mara habari ya jihadi, mpaka, hatimaye baada ya umashuhuri wa *"Mizan ul Hak"* na athari yake yenye sumu, serekali yetu ililazimika mnamo mwaka 1867 kutoa sheria nambari 23 ya mwaka wa 67 kwa kuwazuia mawazo ya kighazi ya makabila ya

mpakani. Sheria hii iliyahusu makabila sita ya mpakani. Na ilitumainiwa sana kwamba kwa sheria hiyo matukio ya mauaji yatakoma. Lakini ni masikitiko kwamba baada ya hapo maandiko makali na machafu ya padre Imadu ud Din wa Amritasar na mapadre wengine wachache wenye midomo michafu yaliharibu sana mapenzi na maelewano ya humu nchini. Kadhalika vitabu vya mapadre wengine, ambavyo hakuna haja ya kuvitaja havikuacha kasoro yoyote katika kupanda mbegu ya uadui nyoyoni. Ilmuradi, watu hao wakaleta madhara sana kwa masilahi ya serekali tukufu. Hatua hii ya serekali yetu yastahili kusifiwa sana kwamba serikali haikuwakataza Waislamu kutoa majibu ya vitabu kama hivyo. Na dhidi ya ukali huo, Waislamu nao wakatumia maneno makali lakini ukali huu ukawa dalili wazi ya moyo mkunjufu wa serekali. Na ufisadi uliotazamiwa kwa sababu ya vitabu vyenye kuaibisha ukakoma ndani kwa ndani kwa sababu ya kuthibitika nia njema na njia ya uadilifu ya serekali hii tukufu. Basi ingawaje tunalazimika kukiri kwa masikitiko kuhusu masheikh wa Islamu kwamba wakifuata swala potofu la jihadi waliyafundisha makabila ya mpakani wawe wanamwaga damu ya maafisa waheshimiwa wa serekali mhisani kwa panga zao, na hivyo waiudhi serekali yao mhisani pasipo hiki, lakini papo hapo

tunawasikitikia ‘masheikh’ wa Ulaya pia ambao ndio mapadre kwamba hao wakawachochea wasioelimika kwa maandishi makali yaliyo kinyume cha ukweli. Kwa kulishutumu mara maelfu swala la jihadi wakahakikishia mioyoni mwa Waislamu wasiostarabika kwamba katika dini yao jihadi ndiyo njia ya kumpatia mtu Pepo haraka sana. Kama hao mapadre walikuwa hawakunuia vibaya nyoyoni, iliwapasa kunyamaa kwa kutambua uhakika ndani kwa ndani kwa kuzilinganisha jihadi za Hadhrat Musa a.s. na Hadhrat Yusha a.s. na jihadi ya Mtume wetu s.a.w. Hata kama tukikubali kwamba waliohimiza kuleta fitina hii ya kuwachokoza watu wa kawaida ndio masheikh wa Kiislamu, bado uadilifu wetu unataulazimu kukiri kwamba kuleta fitina hii maandishi ya mapadre pia yamechangisha kiasi fulani ambayo wayaandikayo mara kwa mara kuwalalamikia Waislamu. Ni masikitiko kwamba baadhi ya majahili baada ya kutenda jambo fulani wanajiweka kando, lakini serekali ya Kiingereza yaikabili matatizo. Kwa kuondoa matatizo hayo, naona shauri bora ndiyo ile iliyoifuata serekali ya Urumi siku hizi, nayo ndiyo hii kwamba kwa kujaribu kila dhehebu likatazwe kabisa kwa miaka michache lisitaje katu kwa uwazi au kwa kudokeza dhehebu jingine katika maandishi yao wala katika hotuba zao. Naam, ipo hiyari ya

kueleza sifa bora za dini yake kadri apendayo. Kwa njia hii itakoma kupanda mbeu za bughudha mpya na zile za zamani zitasahaulika, na watu wataelekea kupendana na kupatana. Na watu wasiostarabika wa mpakani watakapoona kumepatikana baina ya mataifa kusuhubiana na kupendana kiasi hiki basi hatimaye hao nao kwa kuathirika watawahurumia Wakristo namna Mwislamu amhurumiavyo nduguye. Na tadbiri ya pili ni hii kwamba kama masheikh wa Panjab na India kwa kweli wanapinga swala ya jihadi, basi na waandike vijitabu kuhusu habari hii na kuvitafsirisha katika Kipashto na kuvieneza katika makabila ya mpakani. Bila shaka hivyo vitaleta athari kubwa, sharti hayo yote yafanyike kwa moyo wa kweli na jazba na sio kwa unafiki. Amani iwe juu ya wale wanaofuata mwongozo.

Mtangazaji, Mnyeneykevu,
Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau'udi
*Mungu Amsamehe,*
Kutoka Qadian.
Kiliandikwa: 22 Mei 1900

# NYONGEZA YA KIJITABU 'JIHADI'

## *Hakika hasa ya madai ya kuwa Isa Masihi na Muhammad Mahdi, na ombi moja mbele ya Mheshimiwa Viceroy*

Ingawa nimeshaeleza tayari jambo hili katika vitabu vyangu vingi kwamba madai yangu ya kuwa Isa Masihi na pia Muhammad Mahdi hayamaanishi kwamba kwa kweli mimi ni Hadhrat Isa a.s. nami kwa kweli ni Hadhrat Muhammad Mustafaa s.a.w., hata hivyo wale wasiosoma kwa makini vitabu vyangu wanaweza kuingiwa na shaka kana kwamba nimedai nimefanywa hao wawili, na kana kwamba nadai kwamba roho hasa za manabii hao wawili watukufu zimeingia ndani mwangu. Lakini sivyo hivyo, bali hakika hasa ni kwamba kuhusu zama za mwisho manabii wa zamani walitabiri kwamba hizo zitakuwa zama zitakazojaa dhuluma ya aina mbili. Dhuluma moja itazihusu haki za viumbe, na dhuluma ya pili itazihusu haki za Muumba. Kuhusu haki za viumbe dhuluma itakuwa kwamba kwa jina la jihadi wanadamu watamwagwa damu hata kwamba mtu atakayemwua asiye na hatia atadhani kana kwamba kwa mauaji hayo anapata

thawabu kubwa. Na zaidi ya hayo, wanadamu watateswa kwa mateso ya aina nyingi kwa udhuru wa kuwa na ghera ya dini. Basi zama zenyewe ndizi hizi, kwani sawa na imani na uadilifu, kila mcha-Mungu analazimika kukiri katika zama hizi kwamba, kwa mfano, siku zote kabila lisilostaarabika likaalo mpakani linawaua maofisa hao Waingereza ambao ni waliinzi wao au waliinzi wa uhai na heshima za Waislamu walio ndugu zao wa kitaifa; hii ni dhuluma dhahiri namna gani na kuvunja haki za watu! Je, hawakumbuki zama za Makalasinga ambao walikuwa tayari kuua kwa kutolewa adhana ya sala tu. Serekali ya Kiingereza imefanya dhambi gani ambayo kwa sababu yake wanaadhibiwa hivyo wahesimiwa maofisa wake. Serekali hii mara baada ya kuingia katika Panjab iliwatolea Waislamu uhuru kamili katika dini yao. Sasa, si tena zama za kupigwa hata kwa kutoa adhana ya sala kwa sauti ndogo; bali sasa toeni adhana kwa kupanda juu ya minara mirefu. Na misikitini mwenu salini sala za jamaa, hakuna kizuizi. Katika zama za Makalasingia, maisha ya Waislamu yalikuwa kama ya watumwa. Na sasa kwa utawala wa Kiingereza wamepata mara nyingine heshima yao. Uhai, mali na heshima zote tatu ziko salama, milango ya maktaba za Kiislamu

imefunguliwa. Basi, je, serekali ya Kiingereza imefanya wema au imefanya ubaya? Katika zama za Makalasinga makaburi pia ya Waislamu waheshimiwa yalikuwa yanafukuliwa. Tukio la huko Sarhind pia litakuwa halikusahaulika hadi sasa. Lakini serekali hii yalinda makaburi yetu pia kama iwalindavyo wazima wetu. Sisi tunaishi vizuri namna gani chini ya serekali ya heri na amani ambayo haijadhihirisha chuki ya dini hata kidogo. Mwislamu sawa na dini yake afanye ibada, ahiji, atoe zaka, asali au aeleze kwa kutumwa kutoka kwa Mungu kwamba mimi ni mujadidi wa zama hizi, au ni wali, au ni Kutubu au ni Masihi au ni Mahdi, serekali yetu adilifu haina neno, isipokuwa kama yeye mtu huyo akiacha kutii aingiwe na fikara za kuasi. Kisha juu ya wema huu na hisani hizi za serekali, malipo yake yanayotolewa na Waislamu ndiyo kwamba wanawaua maofisa hao pasipo haki, pasipo dhambi, pasipo kosa, ambao wanashughulikia kutumikia nchi usiku na mchana kwa uadilifu. Na kama mkisema watu hao ni wa mpakani; Waislamu wa nchi hii na masheikh wao wanayo dhambi gani, basi jibu lake tunalotoa kwa adabu ni kwamba lazima ipo dhambi, mkitaka mkubali au la. Nayo ndiyo hii kwamba upande mmoja tunapoona katika makabila yasiyostaarabika ya

mpakani shauku ya kuwa ghazi, basi upande wa pili hatuoni katika masheikh wa nchi hii huruma na jazba kwa serikali yao na wakuu wake Waingereza. Kama hao ndio waitakao heri kweli serekali hii tukufu, kwa nini, basi, hawatayarishi fatuwa kwa pamoja na kuieneza katika nchi za mpakani ili udhuru huu wa wajinga hao uondolewe kwamba sisi ni ghazi na tukifa tu tutakwenda Peponi. Mimi siwezi kuelewa kwamba masheikh na wafuasi wao wanadai sana kutii, lakini kwa nini hawawezi kuthibitisha huduma nzuri yoyote. Bali hapo nimelegeza tu waila wapo masheikh wengi pia walio chini ya lawama kubwa zaidi kuliko hiyo. Mungu na Awarekebishe nyoyo zao. Ilmuradi, kuhusu haki za watu dhuluma kubwa yatendeka katika taifa letu la Islamu. Mfalme mhisani atendewapo hivyo, basi watakuwaje wengine! Basi, Mungu akaona kutoka mbinguni dhuluma hii, kwa hiyo kwa kuirekebisha Alimtuma mtu mmoja mwenye tabia ya Hadhrat Isa Masihi a.s., na Akampa jina Masihi kama kivuli cha mtu kionekacho katika maji au kioo kinavyoweza kuitwa kimajazi kuwa mtu huyo. Kwani, mafundisho haya ninayosisitiza — yaani, wapendeni maaudi zenu na watakieni wema kwa jumla viumbe vya Mungu — ndiyo yaliyosisitizwa na yule Nabii mkubwa aliyepita

zamani aitwaye jina Isa Masihi. Na katika zama hizi baadhi ya Waislamu hali yao ndiyo kwamba badala ya kuwapenda maadui zao wanawaua bila haki kwa udhuru wenye aibu wa kidini, watu wasiofanya ubaya wowote, bali wakafanya wema. Kwa hiyo, ilikuwa hakuna budi kwa kurekebisha watu kama hao kwamba aje mtu mmoja akipata ufunuo kutoka kwa Mungu ambaye anayo tabia ya Hadhrat Masihi na amekuja na ujumbe wa suluhu. Je, katika zama hizi haikuwepo haja ya mtu ambaye ndiye mithili ya Isa Masihi? Bila shaka ilikuwepo haja. Kwa kuwa miongoni mwa mataifa ya Kiislamu mamilioni ya watu wanapatikana juu ya uso wa ardhi ambao mazoea yao ni kuwaua watu wa mataifa mengine kwa udhuru wa jihadi — bali baadhi yao, ilhali wanaishi chini ya kivuli cha serekali mhisani, hawawezi kuwapenda kwa ikhlasi kamili, hawawezi kuwa na huruma kamili ya kweli wala hawawezi kuepukana kikamilifu na unafiki — kwa hiyo, ilisikika haja kali sana ya mithili ya Hadhrat Masihi. Basi, mimi ndimi mithili yule niliyetumwa nikifanana na Masihi kiroho, nikiwa na ada na tabia yake.

Na aina ya pili ya dhuluma ambayo anafanyiwa Mwumba, ndiyo itikadi ya Wakristo wa zama hizi kuhusu Mwumba ambayo imepita mipaka yote.

Hakuna shaka ndani yake kwamba Hadhrat Isa a.s. ni nabii mkubwa wa Mwenyezi Mungu. Na bila shaka, Isa Masihi ni mpendwa wa Mungu, mteule wa Mungu, Nuru ya dunia, jua la mwongozo, na aliyemkurubia Mungu na aliyewekwa karibu na Kiti chake cha Enzi. Na mamilioni ya watu wanaompenda kweli na wanafuata maagizo yake na kushikilia miongozo yake, hao watasalimika katika jahanamu. Lakini hata hivyo ni kosa kubwa na kufuru kwamba huyo mteule afanywe kuwa Mungu. Wapendwa wa Mungu huwa na uhusiano mkubwa na Mungu. Kwa sababu ya uhusiano huo kama wajiite 'mwana wa Mungu' au waseme kwamba Mungu ndiye anayesema ndani yao, naye ndiye Anayejionyesha ndani yao, basi maneno haya pia katika hali fulani kwa maana fulani huwa sahihi ambayo yatafumbuliwa. Kwani, mtu akijipoteza katika Mungu na kisha kwa kulelewa kwa nuru yake anapojitokeza upya, basi kumhusu yeye mtu huyo kusema kimajazi kwamba "Huyo siye yeye, bali ni Mungu Aliyedhihiri ndani yake", ndiyo msemo wa kale wa wenye utambuzi wa Mungu. Lakini hiyo haimaanishi kwamba mtu huyo ndiye kweli Mola wa walimwengu. Watu wengi wa kawaida wanapata kuteleza mahali hapa penye hatari, na maelfu ya watawa, mawalii na manabii

waliofanywa Mungu, hao nao kwa kweli wamefanywa kwa sababu ya makosa hayo tu. Ukweli ndio huu kwamba watu wa kawaida wanapoona mambo ya roho na ya mbinguni basi hawawezi kufikia kina chake. Hatimaye kwa kupotosha kidogo na kuchukulia kidhahiri iliyo majazi wanaangukia kosa kubwa na upotevu. Basi, wataalamu wa Kikristo wa siku hizi nao wamenaswa katika kosa hilo hilo, na wanasisitiza Hadhrat Masihi a.s. kwa vyovyote afanywe Mungu. Basi, hii ni kughusubu haki ya Mwumba. Na ili kuimarisha haki hii na kuingiza mioyoni adhama ya Tauhidi, Nabii mmoja Mtukufu amepita huko Arabuni aliyeitwa Muhammad na Ahmad, amani za Mungu zisizohesabika ziwe juu yake. Sheria ilikuwa imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu kubwa ilikuwa: ربّ العالمين

Yaani, Umoja wa Mungu. Na sehemu ya pili ndiyo kwamba wahurumieni wanadamu na watakieni mnayojitakia. Basi, kati ya sehemu hizo mbili Hadhrat Masihi aliisisitiza kuwahurumia wanadamu, maana zama zile zilihitaji usisitizo huo. Na sehemu ya pili iliyo sehemu kubwa yaani:
لااله الا الله iliyo chanzo cha adhma na Tauhidi ya Mungu, akaikazania Hadhrat Muhammad Mteule s.a.w. kwani zama hizo zilihitaji mkazo wa aina

hiyo. Kisha baada yake zimewadia zama zetu ambamo tumo ndani yake sasa. Katika zama hizi makosa hayo mawili yamefikia kileleni. Yaani, kukiuka haki za wanadamu na kuua watu wasio na hatia kuliingia katika itikadi ya Waislamu. Na kwa sababu ya itikadi hii potovu, wasiostaarabika wakawaua maelfu ya wasio na hatia. Na upande wa pili ukiukaji wa haki ya Muumba pia ukafikia kileleni na ukaingia katika itikadi ya Wakristo kwamba Mungu ambaye wanadamu na malaika wanapaswa kumwabudu ndiye Masihi. Na wakazidi kupita mipaka kiasi hiki kwamba ingawa sawa na itikadi yao kuna miungu watatu, lakini kwa kitendo katika dua na ibada ni mmoja tu anayechukuliwa yaani Yesu. Sehemu hizo mbili za ukiukaji wa haki, yaani haki za wanadamu na haki za Mola wa wanadamu, zilikuwa zimefikia kikomo hata kwamba sasa kuna mushkili kupambanua kati ya hizo mbili sehemu ipi imefikia upeo wa mwisho katika kupita mipaka. Basi wakati huu jinsi Mungu Alivyoniita jina Masihi kulingana na ukiukaji wa haki za wanadamu na akanituma nikiwa mithili ya Masihi katika tabia, sifa, khulka na madaha yake, ndivyo Alivyoniita jina Muhammad na Ahmad kulingana na ukiukaji wa haki za Muumba, na ili kueneza Tauhidi akanituma nikiwa mithili ya Hadhrat

Muhammad Mteule s.a.w. Akinipatia tabia, sifa khulka, madaha na kunivisha vazi lake. Basi katika maana hiyo mimi ni Isa Masihi pia na Muhammad Mahdi vile vile. Masihi ni lakabu aliyopewa Hadhrat Isa a.s. ambayo maana yake amgusaye Mungu na ajipatiaye sehemu katika neema ya Mungu na Khalifa wake, na mwenye ikhlasi na ukweli. Na Mahdi ni lakabu aliyopewa Hadhrat Muhammad Mustafaa s.a.w., maana yake aliyeongoka kitabia, mrithi wa miongozo yote, na kivuli kamili cha jina *"Hadi"* (Mwongozi). Basi, fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu imenifanyia mrithi wa lakabu hizo zote mbili katika zama hizi na Amejumuisha lakabu hizo mbili katika dhati yangu. Basi, kwa maana hizo mimi ni Isa Masihi pia na Muhammad Mahdi vile vile. Na mjio huu unaoitwa Buruz katika istilahi ya Kiislamu. Basi nimejaliwa kuwa buruzi mbili: buruzi ya Isa a.s. na buruzu ya Muhammad s.a.w. Ilmuradi, dhati yangu kwa njia ya kuwa buruzi ni mchanganyiko wa sifa za manabii hao wawili. Nikiwa Isa Masih, kazi yangu ni kwamba niwazuie Waislamu kufanya mashambulizi ya kikatili na mauaji. Kama vile katika Hadihi ilivyoelezwa kwa wazi kwamba Masihi atakapokuja duniani mara ya pili, atakomesha vita vyote vya kidini, ndivyo hivyo inavyoendelea

kufanyika. Hadi tarehe ya leo Jumuiya ya watu karibu elfu thelathini au kidogo zaidi wapo pamoja nami[11] ambao wanaishi katika sehmeu mbali mbali za India inayotawaliwa na Uiingereza. Na kila mtu anayejiunga nami na kuniamini kuwa Masihi Mau‘udi, kuanzia siku hiyo analazimika kuwa na itikadi hii kwamba katika zama hizi jihadi ni haramu kabisa, kwani Masihi amekwisha fika. Hasa kulingana na mafundisho yangu analazimika kuitakia serikali ya Kiingereza heri kwa moyo wa kweli, wala sio kiunafiki. Na hii ndiyo bendera ya suluhu iliyotwekwa; hata kama masheikh laki moja wangetaka kuanzisha mpango wenye athari kama huu ili kuzuia jihadi za kikatili isingeyumkinika kwao. Nami natarajia, Mwenyezi Mungu Akipenda, katika miaka michache tu jumuiya hii ibarikiwayo na ipendayo amani ambayo inaendelea kufuta mawazo ya jihadi na ughazi, itaongezeka hadi laki kadha, ndipo wafanyao jihadi ya kikatili watabadilika mawazo.

Na nikiwa Muhammad Mahdi, kazi yangu ndiyo

[11]Ijapokuwa watu mahsusi wenye elimu na busara sana watakuwa karibu elfu kumi, lakini watu wa kila aina ambao kati yao wapo pia wasiojua kusoma na kuandika, sio kidogo kuliko elfu thelathini, bali pingine wanazidi. Mwandishi.

kuimarisha duniani tena Tauhidi ya Mungu kwa ishara za mbinguni, kwani Sayyedna na Maulana Hadhrat Muhammad Mustafaa s.a.w. aliimarisha adhama, nguvu na kudura ya Mungu mioyoni mwa waabudu masanamu wa Arabuni kwa kuonyesha ishara za mbinguni. Kadhalika nami nimesaidiwa na Roho Mtakatifu. Yule Mungu ambaye Aliendelea kudhihiri kwa manabii wote, na Akadhihiri kwa Musa Kalimullah huko Turi na Akamwondokea Hadhrat Masihi mlimani Seiri na Akaangaza kwa Hadhrat Muhammad Mustafaa s.a.w. katika kilima cha Parani, ndiye huyo huyo Mungu Mweza Mtakatifu Amenidhihirikia, Akaongea nami na Akaniambia kwamba Yule Mtukufu ambaye manabii wote walitumwa kwa ibada yake, ndiye Mimi, Mimi peke yangu ndimi Muumba na Mmiliki na hakuna mshirika wangu, nami nimeepukana na kuzaliwa au kufa. Na imefafanuliwa kwangu kwamba itikadi ya Wakristo wengi wa dunia kuhusu Masihi, yaani utatu na kafara na kadhalika, haya yote ni makosa ya kibinadamu na ni kuachana na mafundisho sahihi. Mungu Amenijulisha moja kwa moja kwa Neno lake hai na Ameniambia kwamba kama ukikabili tatizo kwamba watu wanasema tuelewaje kwamba umetokana na Mungu, basi waambie kwamba juu yake dalili hii inatosha

kwamba ishara zake za mbinguni ni mashahidi wangu, maombi yanakubaliwa, habari za ghaibu zaelezwa kabla hazijatokea, na siri zile asizojua yeyote isipokuwa Mungu, zinadhihirishwa kabla hazijadhihirika. Na ishara ya pili ndiyo hii kwamba kama mtu akitaka kushindana nami katika mambo haya: kwa mfano, kukubaliwa dua fulani na kujulishwa mapema kwamba hiyo imekubaliwa, au kujua mambo ya ghaibu yanayozidi kikomo cha elimu ya mtu, basi huyo atashindwa katika mashindano haya, hata akiwa wa Mashariki au wa Magharibi. Hizo ndizo ishara nilizopewa mimi, ili kwa njia hizo niwawute watu kwenye Mungu wa kweli aliye Mungu kwa hakika wa roho zetu na miili yetu, ambaye kila mmoja atasafiri kwake siku moja. Hii ni kweli kwamba dini ile si kitu isiyo na nguvu ya Mungu. Manabii wote wamesema kuwa alama ya dini ya kweli ndiyo hii tu kwamba dini hiyo iwe na nguvu ya Mungu. Jambo hili pia linapaswa kukumbuka kwamba majina yote hayo mawili Aliyonipatia Mungu siyo tangu siku chache tu, bali katika kitabu changu *Barahin-e-Ahmadiyya* kilichochapishwa miaka ishirini hapo kabla, nimeitwa majina hayo mawili katika ufunuo wa Mwenyezi Mungu — yaani, Isa Masihi na Muhammad Mahdi — ili niwafikishie makundi

haya mawili ya Waislamu na Wakristo ujumbe nilioeleza hapo juu. Laiti mioyo ingetafuta ukweli na ingeiogopa siku ya mwisho, basi kila mtafuta ukweli alikwishapewa nafasi ya kujipatia utulivu kwangu. Dini ya kweli ndiyo dini iliyo na nguvu ya Mungu ndani yake na inaonyesha uso wa Mwenyezi Mungu kwa kazi za kimwujiza. Basi, mimi ni shahidi wa jambo hili kwamba dini kama hiyo ndiyo dini ya Tauhidi iliyo Uislamu ambamo kiumbe hakupewa daraja la Muumba. Na dini ya Kikristo pia ilikuwa imetoka kwa Mungu, lakini nasikitika kwamba sasa haikubakia juu ya mafundisho yale. Na pia nawasikitikia Waislamu wa zama hizi kwamba wamejinyima sehemu ya pili ya sheria ihusikanayo na huruma ya wanadamu, upendo na huduma yao, na wakiisha dai Tauhidi, bado wameshikwa na khulka za kikatili zilizo aibu. Nilijaribu mara nyingi kuwatenganisha na mazoea yao hayo, lakini nasikitika kwamba wanapatwa na baadhi ya mambo ya kuwachochea yanayoamsha jazba zao za kinyama, nayo ndiyo maandishi ya baadhi ya mapadre wenye busara ndogo, yanayoathiri kama sumu, kwa mfano, vitabu vya padre Imaduddin, na vitabu vya padre Thakardas, na vitabu vya Safdar Ali, na kitabu cha *Ummahatul Muminin*, na kijitabu cha padre Riwari, vilivyojaa maneno ya

kumvunjia sana Mtume wetu s.a.w. heshima na kumkadhibisha. Hivyo ni vitabu ambavyo mtu yeyote miongoni mwa Waislamu atakayevisoma mara atapandwa na hasira kama hana subira na uvumilivu wa hali ya juu. Kwani, katika vitabu hivyo badala ya maelezo ya kielimu kuna matusi zaidi ambayo Waislamu wa kawaida hawawezi kustahamili. Padre mmoja mwenye kuheshimika anaandika katika gazeti lake lililokuwa linatolewa huko Lacknow kwamba kama (uchafuzi wa) mwaka 1857 unawezakana kutokea tena, basi huo utachochewa na vitabu vya padre Imaduddin. Sasa yafaa kufikiria kwamba maneno ya padre Imaduddin ni hatari namna gani ambayo kuhusu hayo padre mmoja mheshimiwa anaeleza rai hiyo. Hivi majuzi mimi nami nilipoona hasira baina ya Waislamu kwa sababu ya maandishi kama hayo, nikatoa mara chache majibu makali kidogo kimaandishi ya vitabu hivyo vyenye maneno makali. Kwa maandishi hayo nilikusudia hasira ya Waislamu ipoe kwa sababu ya pigo kwa pigo. Basi ingawa kwa maandishi yenye hekima hii Waislamu walifaidika na kwa kupata jibu la aina hii wakatulia, lakini titizo ni kwamba bado mapadre wanatoa mara kwa mara maandishi ambayo Waislamu wenye kukasirika haraka na wenye tabia kali hawawezi kuvumilia. Hii ni kazi

ya hatari sana kwamba Mapadre upande mmoja wanawasingizia Waislamu kwamba katika Kurani wameamrishwa kupigana jihadi siku zote na katika kila zama, kana kwamba hao wanaendelea kuwakumbusha desturi ya jihadi, na tena kwa kueneza maandishi makali wanaendelea kuwachokoza. Sijui watu hao ni majuha gani ambao hawazingatii kwamba kwa kuunganisha mbinu hizo mbili matokeo ya kutisha yaweza kutokea. Tumeshaandika mara nyingi kwamba Kurani Tukufu haifundishi kabisa jihadi hiyo. Hakika yenyewe ndiyo hii tu kwamba katika siku za mwanzo baadhi ya wapinzani walitaka kuzuia Islamu kwa upanga, bali kuiangamiza, basi Islamu iliwainulia upanga kwa kujilinda; na kuhusu hao tu iliagizwa wauawe au wasilimu. Basi amri hiyo ilikuwa mahususi kwa zama zile, haikuwa kwa sikuzote. Na Islamu haidhamini matendo ya wafalme yaliyofanyika kwa sababu ya makosa matupu au uchoyo baada ya zama za Mtume s.a.w. Sasa yule mtu ambaye anawakumbusha mara kwa mara Waislamu wasio na ujuzi swala la jihadi kwa kuwadanganya, yeye mtu huyo kana kwamba anataka kuchochea mazoea yao yenye sumu. Ingekuwa afadhali kama mapadre wakizingatia matukio sahihi ya historia wangesisitiza kwamba katika Islam hakuna jihadi, wala hakuna

amri ya kusilimisha kwa kutumia nguvu. Kitabu ambamo mpaka sasa aya hii imo kwamba

لَآ اِكۡرَاهَ فِى الدِّيۡنِ ۙ[12]

— yaani, katika dini karaha haitakikani — je, kuhusu hicho tunaweza kudhani kwamba kinafundisha jihadi? Ilimuradi, hapa tuwalalamikieje masheikh! Bali tunawalalamikia mapadre wenyewe kwamba hawakushika njia iliyokuwa sahihi kweli na iliifaa serikali masilahi yake!! Kwa uchungu huo nilimwomba Mheshimiwa Kaimu wa Mfalme (Viceroy) mara mbili kwamba kwa muda fulani mtindo huu wa majadiliano wa kundi moja kukosoa dini ya kundi lingine ukomeshwe; lakini mpaka sasa maombi hayo hayajaangaliwa. Hivyo, sasa mara ya tatu namwomba Mheshimiwa tena kwamba njia hii ya kuzishambulia dini zingine ipigwe marufuku kwa miaka mitano kwa akali, na ikataliwe kabisa kwamba kundi moja lisishambulie katu kupinga itikadi za kundi lingine. Kwani, kwa sababu hiyo unafiki unaendelea kuzidi nchini siku hadi siku, mpaka vikao vyao kirafiki vya makundi mbali mbali vimekoma. Kwani wakati mwingine kundi moja linapata kulipinga kundi jingine kwa

[12] Al-Baqara, 2:257

upungufu wake wa ujuzi na upinzani huo kwa kweli hauwi sahihi na unahuzunisha sana mioyo, na pengine unazusha fitina, kama vile kuwashutumu Waislamu kuhusu jihadi. Bali, upinzani kama huo ukilikumbusha kundi la pili unazindua ile hamaki iliyokuwa imesahaulika na hatimaye unasababisha ufisadi. Basi, kama serekali yetu yenye busara iunde sheria hii kwa miaka mitano kwamba wafuasi wa madhehebu yote ya India iliyo chini ya serikali ya Kiingereza, pamoja na mapadri, wakatazwe kabisa wasishambulie katu dini zingine, bali wakutane kwa mapenzi na hulka. Na kila mtu aeleze uzuri wa dini yake, hapo nayakini kwamba mmea huu wenye sumu wa mafarakano na chuki unaoendelea kukua ndani kwa ndani utatokomea haraka sana. Na kazi hii ya serekali ikipata sifa bila shaka italeta athari (njema) juu ya watu wa mpakani pia, na yatadhihirika matokeo ya amani na suluhu. Huko mbinguni nako utashi wa Mungu unaoonekana ni kwamba njia za vita na mapigano zikome, na njia za suluhu na kupendana zipate kufunguliwa. Kama kuna ukweli fulani katika dini moja basi, ukweli huo unafaa udhihirishwe; haifai kuendelea kuzitolea aibu dini zingine. Pendekezo hili ninalotoa kulifuata au kulikubali si kazi ya kila mtawala; ni jukumu la watawala wenye

busara kubwa kwamba waelewe uhakika huu. Nasi tunategemea kwamba mheshimiwa kaimu wa Mfalme (Viceroy) Bwana Curzon lazima ataangalia ombi hili kwa sababu ya hulka kunjufu na hekima, kwa hima yake ya kifalme atalifanya pendekezo hili litekelezwe. Na kama sivyo, basi katika enzi yake njema achukue hatua kwa ajili ya Mungu ajaribu kuchunguza kwamba ni dini ipi kati ya dini zilizopo katika nchi hii ambayo ina nguvu ya Mungu. Yaani, wanavyuoni maarufu wote wa Waislamu, Waaria, Makalasinga, Wasanatan Dharm, Wakristo, Wabarhamu, Mayahudi na wengineo waagizwe kwamba kama kuna nguvu ya Mungu katika dini yao, ikiwa kwa sura ya utabiri au kwa sura nyingine, basi na waionyeshe. Kisha ikithibitika kwamba nguvu hiyo adhimu iliyo Nguvu Tukufu imo katika dini fulani, basi, dini hiyo iheshimiwe na kukubaliwa kuwa ya kweli. Na kwa kuwa nimejaliwa roho kutoka mbinguni kwa kazi hii, kwa hiyo kwanza kabisa kwa niaba ya Jumuiya yangu nzima najitokeza kuleta ombi kwamba niko tayari kwa mtihani huo kushindana na makundi mengine. Na pamoja na hayo naomba dua kwamba Mwenyezi Mungu daima Aistawishe serekali yetu hii ambayo chini ya kivuli chake nimepata nafasi kwamba nikiwa nimetoka kwa Mungu nipeleke

maombi kama haya ili kudhihirishia utukufu wa Mungu. Wassalam, 7 Julai 1900

Mwombaji, mnyenyekevu
Mirza Ghulam Ahmad
Kutoka Qadian.

---